TANGAZO LA SERIKALI Na. 664 la tarehe. 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA MJIMWEMA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Mjimwema ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Mji wa Makambako.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye njia panda ya barabara ya Njombe – Songea na bomba la Mafuta la Tanzania – Zambia - Mafuta (TAZAMA) kwenye alama yenye majira – nukta 700553E, 9021369N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya Njombe – Songea hadi njia panda ya Soko la Mbao kwa umbali wa kilomita 1.539 hadi alama yenye majira – nukta 700415E, 9019870N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki karibu na makaburi ya Magegere kwa umbali wa kilomita 0.993 hadi kwenye alama yenye majira – nukta 701365E, 9019584N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini Mashariki kwa kufuata barabara ya Mpakani kwa umbali wa kilomita 0.669 hadi kwenye kalavati kwenye alama yenye majira - nukta 701624E, 9020199N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Mashariki kwa kufuata eneo oevu kwa umbali wa kilomita 0.643 hadi bonde la Luligo kwenye alama yenye majira - nukta 702065E, 9020652N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 1.097 hadi kwenye alama yenye majira – nukta 701463E, 9021506N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.506 kuelekea bomba la mafuta la TAZAMA hadi kwenye alama yenye majira – nukta 701071E 9021787N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kuelekea bomba la mafuta la TAZAMA kwa umbali wa kilomita 0.687 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*